



TAHARA NA SALAH

**SHEIKH MUHAMMAD AL'UTHAIMIN
MFASIRI
SULAYMAN A. S. SHAQSSY**

الطهارة والصلوة

تأليف فضيلة الشيخ: محمد بن صالح العثيمين

لِكُشْتَ الْعَاقِي لِلرَّدِّ عَوْكَةٍ وَلَا إِشَادَةٍ وَلَا مُعَادَةٍ فَإِنْ أَرْجَمْتَ

الطهارة والصلوة

Yaliyomo

Idhini ya Mwandishi	1
Utangulizi	2
Udhu, Josho Kubwa (Al-Ghusl) na Salah	3—10
Mambo yaliyo Makruhu kufanywa katika Salah	10—12
Anavyojitaharisha Mgonjwa	13—15

فضيلة الشيخ:

محمد بن صالح العثيمين

حفظه الله ورعاه

السلام عليكم ورحمة الله وبركاته، وبعد . . .

يطيب لنا أن نقدم بين أيديكم ترجمة لكتابكم الطهارة والصلوة باللغة السواحلية، وهي إحدى اللغات الحية في القارة الأفريقية ولما للكتاب من أهمية في حياة المسلمين فلقد قام بعض المؤثوق بهم من طلبة العلم بدولة كينيا بترجمته، مع العلم أنه قد تمت مراجعته من بعض طلبة العلم المتخريجين من جامعة الإمام محمد بن سعود الإسلامية.

هذا نأمل من فضيلتكم السماح لنا بطباعة الكتاب ونشره بين المسلمين.

وجزاكم الله خيراً، وجعله في ميزان حسناتكم.

إبنكم /

د. عادل بن محمد السليم

أمين عام المنتدى الإسلامي

بسم الله الرحمن الرحيم
جم - وعليكم السلام ورحمة الله وبركاته
اسمح لكم بطبع كتابي (الطهارة والصلوة) باللغة السواحلية
بشرط العناية بتصحيحه ومراجعته بروفته قبل طبعه
من ذوى الافهام. كتبه محمد الصاحب العثيمين في ٢٦/١١/١٤١٦

محمد العثيمين

Utangulizi

Risala za Twahara na Swala zimeandikwa na Sheikh Mohammad Bin Swaleh Al-Uthaimin.

Mwanachuoni huyu ni mionganini mwa wanazuoni mashuhuri katika ulimwengu wa kiiislamu na ni mwaandishi aliyeandika vitabu vingi kwa lugha ya kiarabu kwa ajili ya kueneza ilimu na maarifa. Tumeonelea kutafsiri risala hizi muhimu kwa lugha ya kiswahili ili wasomi wa lugha hii waweze kufaidika na maarifa na ujuzi wa mtaalamu huyu.

Mfasiri wa risala hizi Sheikh Swaleh Shaqsy ni maarufu sana baina ya waandishi na wafasiri walioko katika Afrika Mashariki kwa uandishi wake na vitabu vyake vimejaa masokoni .

Sina budi kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu (S.W.T.) kisha kwa mwaandishi na pia mfasiri na mwisho ni kwa Al-Muntada Al-Islami Trust kwa kukubali kugharamia uchapishaji wa kitabu hiki ambacho tunatarajia kitakuwa ni muongozo mzuri kwa kila anaetaka kufuata nyayo za bwana Mtume Muhammad (S.A.W.) katika kutekeleza ibada kama aliviyotufundisha bila uzushi wowote.

Haki ya kunakili imehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigisha chapa au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi au namna yoyote ile bila ya idhini

Babake Hamza
Abubakar. A. Abubakar
14/2/1416h
12/7/1995

Udhu, Josho Kubwa (Al-Ghusl) na Salah

Sifa zote njema na shukrani zote za dhati ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu. Sala na salamu zimshukie Mtume wa mwisho ambaye ni kiongozi wa wacha-Mungu na Sayyidi wa viumbe wote, yeze ni Mtume wetu Muhammad; pia ziwafikie Aali zake na Sahaba zake wote.

Amma Ba'd: Asema Muhammad ibn Al-'Uthaimin mjaa fakiri kwa Mwenyezi Mungu (s.w.): "Hii ni Risala fupi katika mambo ya Udhu, Josho kubwa (Al-Ghusl) na Salah kwa mujibu wa yaliyokuja katika Qur'an na Sunnah."

Udhu

Udhu: Ni tahara iliyowajibishwa ili kujitakasa kutokana na hadathi ndogo kama vile mkojo, choo, kujamba, usingizi mzito na kula nyama ya ngamia.

Jinsi ya kutawadha

1. Anuie moyoni kukusudia kutawadha bila ya kuitamka hiyo nia, kwa vile Mtume (s.a.w.) hakuwa akitamka nia katika kutawadha kwake, wala katika kusali kwake, wala katika tendo lolote mionganini mwa 'ibada zake; na sababu ni kuwa Mwenyezi Mungu ayajuwa vema yote yaliyomo moyoni, basi imekuwa hamna haja ya kumjulisha (s.w.) yaliyomo humo moyoni.
2. Kisha aseme: *Bismillah* بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
3. Kisha auoshe mikono yake mara tatu.
4. Kisha asukutue na kuvuta maji puani na kuyatoa mara tatu.
5. Kisha aoshe uso wake mara tatu, kwa upana: toka sikio hadi sikio; na kwa urefu: kutoka maoteo ya nywele juu ya paji la uso hadi kidevuni.
6. Kisha aoshe mikono yake mara tatu toka mwanzo wa vidole hadi vifundoni, na aanze na wa kulia kisha wa kushoto.
7. Kisha apake kichwa chake mara moja kwa mkono wake wenye unyevunyevu wa maji: apake kutoka mbele ya kichwa hadi nyuma yake kisha afike tena alipoanzia.
8. Kisha aoshe masikio yake mara moja kwa pamoja akitumia vidole vyake vya shahada ndani ya masikio na vidole gumba nje ya masikio.
9. Kisha aoshe miguu yake mara tatu, kutoka mwanzo wa vidole hadi vifundoni, akianza mguu wa kulia na kumalizia wa kushoto.

Josho Kubwa (al-Ghusl)

Hii ni tahara ya wajibu ya kujitaharisha kutokana na hadathi kubwa kama vile janaba na hedhi.

Jinsi ya Kuoga Josho Kubwa

1. Anuie kuoga josho kubwa, kimoyomoyo tu bila kuitamka nia.
2. Kisha aseme: *Bismillah*
3. Kisha atawadhe udhu kamili.
4. Kisha amwagie maji kichwani hadi kikisha loa akieneze maji chote mara tatu.
5. Kisha aoshe kiwiliwili chake chote.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kutayammam

Tayammum ni tahara ya wajibu kwa kutumia mchanga, nayo ni badili ya udhu na ghusli kwa ambaye hakupata maji au akiyatsumia yatamdhuru.

Jinsi ya kutayammam

Anuie kuwa anatayammam badili ya udhu au ghusli, kisha apige viganja vyake ardhini au chochote chenye vumbi kama vile viambaza, kisha apake uso na mikono yake.

Salah

Salah: Ni ‘ibada yenye maneno na vitendo; mwanzo wake ni *Takbiratul-Ihram* na mwisho wake ni salamu.

Na Muislamu anapotaka kusali anawajibika kutawadha ikiwa ana hadathi ndogo, au kuoga ikiwa ana hadathi kubwa, au atayammam asipopata maji au yatamdhuru ayatumia. Mwili wake, nguo zake na mahala pa kusalia pawe nadhifu.

Jinsi ya kusali

1. Aelekee qibla kwa mwili wake wote bila ya kupotoka wala kugeuka.
2. Kisha anuie Salah anayotaka kusali—kimoyomoyo bila kutamka nia.
3. Kisha alete *Takbiratul-Ihram* kwa kusema:

Allahu Akbar

Yaani:

الله أكْبَر

“Mwenyezi Mungu ndiye Mkubwa kuliko wote”, na ailetapo hiyo *Takbir* ainue mikono usawa wa mabega yake.

4. Kisha aikunje mikono yake kifuani kwa kuuweka wa kulia juu ya wa kushoto.
5. Kisha asome *Du‘aul-Istiftah*:

اللَّهُمَّ بَاعْدِ بَنِي وَبَيْنَ خَطَايَايِي كَمَا بَااعْدَتْ بَيْنَ الْمَشْرَقِ وَالْمَغْرِبِ . اللَّهُمَّ
نقِنِي مِنْ خَطَايَايِي كَمَا يُنقِنُ النُّوبَ الأَبْيَضَ مِنَ الدَّنَسِ . اللَّهُمَّ اغْسلِنِي
مِنْ خَطَايَايِي بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرْدِ

Allahumma ba'id bainy wa baina khatayay kama ba'adta bainal-mashriqi wal-maghrib. Allahumma naqqiny min khatayay kama yunaqqath-thawbul-abyadhu minad-danasi. Allahumma aghsilny min khatayay bil-mai waththalji wal-barad.

Yaani:

“Ewe Mola wangu! Niepushe mimi na makosa yangu kama Ulivyobaidisha baina ya mashariki na magharibi. Ewe Mola wangu! Nitakase mimi kutokana na makosa yangu kama inavyonadhifishwa nguo nyeupe kutokana na uchafu. Ewe Mola wangu! Nioshe mimi kwa maji na theluji na baridi kutokana na makosa yangu.”

Au aseme:

سبحانك اللهم وبحمدك، وتبarak اسمك، وتعالى جدك، ولا إله غيرك

Subhanakal-Lahumma wa bihamdika, wa tabarakasmuka, wa ta'ala Jadduka, wa la ilaha ghayruk.

Yaani:

“Umetukuka Ewe Mola wangu! Sifa njema zote na shukrani za dhati zote ni Zako! Limebarikiwa Jina Lako! Umetukuka Ufalme Wako! Na hapana Mola ila Wewe tu!”

6. Kisha ajilinde kwa Mwenyezi Mungu kwa kusema:

أعوذ بالله من الشيطان الرجيم
A'udhu bil-Lahi minash-shaytanir-rajym.

7. Kisha apige Bismillahi na kusoma Suratal-Fatihah:

**بسم الله الرحمن الرحيم . الحمد لله رب العالمين . الرحمن الرحيم .
مالك يوم الدين . إياك نعبد وإياك نستعين . إهدنا الصراط
المستقيم . صراط الذين أنعمت عليهم غير المغضوب عليهم ولا الضالين**

*Bismillahir-Rahmanir-Rahim * Alhamdu lil-Lahi Rabbil-'Alamin * Ar-Rahmanir-Rahim * Maliki Yaumid-Dyn * Iyyaka na'budu wa Iyyaka nasta'in * Ihdinas-Siratal Mustaqim * Siratal-ladhina An'amta 'alayhim ghairil-maghdihi 'alayhim waladh-dhalyn**

Yaani:

“Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

“Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengi wote.

“Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

“Mwenye kumiliki Siku ya Malipo.

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu, na Wewe tu Ndiye tunayekuomba msaada.

“Tuongoze njia iliyonyoka.

“Njia ya wale Uliowaneemesha; siyo (ya wale waliokasirikiwa), wala (ya) wale waliopotea.”

Kisha aseme: *Amin*

آمين

Yaani: “Ewe Mola! Tukubalie!”

8. Kisha asome sehemu ya Qur’ani kiasi atakachojaaliwa.
9. Kisha arukuu, yaani aupinde mgongo wake kwa kumtukuza Mwenyezi Mungu. Aiendeapo rukuu aseme:
Allahu Akbar hali amenyanya mikono yake usawa wa mabega yake. Na ni sunna katika rukuu mgongo wake unyooke sawasawa, kichwa chake kiinuke usawa wa kiuno chake, na aweke mikono juu ya magoti yake hali amevichanua vidole vyake.

10. Aseme mara tatu katika kurukuu kwake:

Subhana Rabbiyal-‘Adhym سُبْحَانَ رَبِّ الْعَظِيمِ ثَلَاثٌ مَرَاتٌ

Yaani: “Ametakasika Mola wangu Mtukufu na sifa zote za upungufu.”

Ni vema pia akiongeza: سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي

Subhanakal-Lahumma wa Bihamdika, Allahumma ghfirly.

Yaani:

“Umetukuka Ewe Mola wangu! Sifa njema zote na shukrani zote za dhati ni Zako. Ewe Mola nighufirie.”

11. Kisha ainuke kutoka katika rukuu huku asema:

Sami‘al-Lahu liman Hamidah سمعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمَدَهُ

Yaani: “Mwenyezi Mungu anamsikia kila anayemshukuru.”

12. Kisha aseme baada ya kuinuka:

رَبِّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ . مِنْ السَّمَاوَاتِ وَمِنْ الْأَرْضِ وَمِنْ مَا شَتَّى مِنْ شَيْءٍ بَعْدَ

Rabbana wa Lakal-hamd mil' as-samawati, wa mil'al-a radhi wa mil'a ma Shi'ta min shay'in ba'd

Yaani: “Ewe Mola wetu! Sifa njema na shukrani za dhati zote ni Zako

ujazo wa mbingu na ujazo wa ardhi, na ujazo wa chochote kitakachokuridhisha baada ya hivyo.”

13. Kisha asujudu kwa ajili ya kumnyenyeka Mwenyezi Mungu: hii ni sijda ya kwanza ambapo katika kuiendea atasema:

Allah Akbar

الله أكبر

Yatakikana asujudu juu ya viungo vyake saba: paji la uso pamoja na pua, viganja vyake viwili, magoti yake mawili na vidole nya miguu yake miwili. Aiepushe mikono isiguse mbavu zake, wala asiilaze mikono yake ardhini, na vichwa nya vidole vyake nya miguu vielekee qibla.

14. Aseme mara tatu katika kusujudu kwake:

Subhana Rabbial-A'la

سبحان رب الأعلى

Yaani: “Ametakasika Mola wangu na sifa zote za upungufu.”

Na ni vyema akiongeza:

سْبَحَنَكَ اللَّهُمَّ رَبُّنَا وَبِحَمْدِكَ، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي

Subhanakal-Lahumma Rabbana wa Bihamdika, Allahumma ghfirly.

Yaani:

“Umetukuka Ewe Mola wetu, na sifa njema zote ni Zako! Ewe Mola wangu! Nighufirie.”

15. Kisha ainuke kutoka katika sijda huku asema:

Allahu Akbar

الله أكبر

16. Kisha akae kitako baina ya sijda mbili juu ya mguu wake wa kushoto hali ya kuusimamisha mguu wake wa kulia, na aweke mkono wake wa kulia karibu na goti, akunje kabisa kidole chake kidogo cha mwisho na kinachofuatia hali ya kukinyosha kidole chake cha shahada ambacho atakingisha wakati wa kusoma du'a, hali ya kuwa kidole gumba mwisho wake umegusana na mwisho wa kidole chake cha kati-hivyo viwili vikunda mduara. Na auweke mkono wake wa kushoto juu ya paja la kushoto hali ya kuvikunjua vidole vyake mwishoni mwa hilo paja karibu na goti.

17. Aseme katika kikao chake baina ya sijda mbili:

رب اغفر لي وارحمني واهدني وارزقني واجبرني وعافني

Rabbi ghfirly warhamny wahdiny warzuqny wajburny wa 'afiny.

Yaani:

“Ewe Mola wangu! Nighufirie, Nihurumie, Niongoze, Niruzuku, Nitengezee yaliyoniharibikia na Nijaalie afya.”

18. Kisha asujudu kwa unyenyekevu sijda ya pili: aseme na afanye yale yale aliyoafanya katika sijda ya kwanza na aiendee hiyo sijda ya pili kwa kusema:

Allahu Akbar

الله أَكْبَر

19. Kisha ainuke kutoka katika hiyo sijda ya pili akisema:

Allahu Akbar

الله أَكْبَر

Na aiendee rakaa ya pili na humo aseme na afanye yale yote aliyoafanya katika rakaa ya kwanza isipokuwa hasomi *Du'aul-Istiftah*.

20. Kisha akae baada ya kumaliza sijda ya pili huku akisema:

Allahu Akbar

الله أَكْبَر

Na akae sawasawa kama alivyokaa baina ya sijda mbili.

21. Na katika kikao hiki asome *Tashahhud*:

التحيات لله والصلوات والطيبات . السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته . السلام علينا وعلى عباد الله الصالحين،أشهد أن لا إله إلا الله وأشهد أن محمداً عبده ورسوله. اللهم صل على محمد وعلى آل محمد، كما صليت على إبراهيم وعلى آل إبراهيم إنك حميد وبارك على محمد وعلى آل محمد، كما باركت على إبراهيم وعلى آل إبراهيم إنك حميد مجيد. أعود بالله من عذاب جهنم ، ومن عذاب القبر، ومن فتنة المحي والممات ، ومن فتنة المسيح الدجال

Attahiyyatu lil-Lah, was-Salawatut-Tayyibat. Assalamu 'alayka ayyuhan-Nabiyyu wa Rahmatullahi wa Barakatuh. Assalamu 'alayna wa 'ala ibadil-Lahis Salihin. Ash-hadu an la ilaha illal-Lah, wa ash-hadu anna Muham-madan 'abduhu wa Rasuluh. Allahumma Salli 'ala Muhammadin wa 'ala Aali Muhammadin, kama sallayta 'ala Ibrahima wa 'ala aali Ibrahima Innaka Hamidun Majid. Wa barik 'ala Muhammadin wa 'ala Aali Muhammadin kama barakta 'ala Ibrahima wa 'ala aali Ibrahima Innaka Hamidun Majid. A'udhu Billahi min 'adhabi Jahannam, wa min 'adhabil-qbr, wa min fitnatil mahya wal-mamat, wa min fitnatil-masihad-Dajjal.

Yaani:

“Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu, vile vile rehema na

mazuri yote hutupatia Mwenyezi Mungu. Amani ya Mwenyezi Mungu ikuteremkie Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu pamoja na rehema na baraka Zake. Nasi pia itushukie amani ya Mwenyezi Mungu pamoja na waja Wake wema wote: Nakiri kuwa hakuna Mola ila Mwenyezi Mungu, na nakiri kuwa Muhammad ni mja Wake na ni Mjumbe Wake. Ewe Mwenyezi Mungu! Mpe rehema Mjumbe Wako Muhammad na wafuasi wake Nabii Muhammad, kama Ulivyompa rehema Nabii Ibrahim na wafuasi wake Nabii Ibrahim. Wewe Ndiye Unayestahiki kuhimidiwa na viumbe vyote na Ndiye Mwenye Utukufu. Na Umbariki Nabii Muhammad na wafuasi wake Nabii Muhammad kama Ulivyombariki Nabii Ibrahim na wafuasi wake Nabii Ibrahim. Wewe Ndiye Unayestahiki kuhimidiwa na viumbe vyote, na Ndiye Mwenye Utukufu. Ewe Mola wangu! Mimi najilinda Kwako kutokana na ‘adhabu ya Jahannam, na kutokana na ‘adhabu ya kaburi , na kutokana na fitna ya uhai na mauti na kutokana na fitna ya Masihid-Dajjal.”

Kisha amwombe Mola apendayo mionganoni mwa kheri za dunia na Akhera.

22. Kisha atoe salamu: Kwanza kuliani akisema:

Assalamu 'alaykum wa Rahmatullah **السلام عليكم ورحمة الله**
na mwishowe kushotoni hivyo hivyo.

23. Na ikiwa Salah ni ya rakaa tatu au nne atakomea pale inapoishia *Tashahhud* ya kwanza napo ni katika maneno haya:

أشهد أن لا إله إلا الله وأشهد أن محمداً عبده ورسوله

Ash-hadu an la ilaha illal-Lah wa ash-hadu anna Muhammad 'abduhu wa Rasuluh.

Yaani:

“Nakiri kuwa hakuna Mola ila Mwenyezi Mungu, na nakiri kuwa Muhammed ni mja Wake na Mjumbe Wake.”

24. Kisha ainuke wima hali ya kusema: *Allahu Akbar* **الله أكبر**
huku ameinua mikono yake usawa wa mabega yake.
25. Kisha aisali sehemu iliyobaki katika Salah yake jinsi alivyoisali rakaa ya pili isipokuwa hasomi ila Al-Fatihah.

26. Kisha akae juu ya tako lake la kushoto hali ameusimamisha mguu wake wa kulia, na mguu wake wa kushoto umejitokeza chini ya muundi wake wa kulia, na mikono yake iwe juu ya mapaja yake, kama alivyoiweka katika *Tashahhud* ya kwanza.

27. Katika kikao hiki aisome *Tashahhud* yote.

28. Kisha atoe salamu kuliani:

السلام عليكم ورحمة الله

Assalamu 'alaykum wa Rahmatullah na kushotoni hivyo hivyo.

MAMBO YALIYO MAKRUHU KUFANYWA KATIKA SALAH

1. Yachukiza kugeuza kichwa au macho katika Salah; ama kuangalia mbinguni ni haramu.
2. Yachukiza kuleta mchezo katika Salah au kusogezasogea viungo vya mwili.
3. Yachukiza kubeba kitu kizito katika Salah ambacho chashughulisha mawazo; au kitu cha rangi rangi chenye kuvutiza macho kukiangalia.
4. Yachukiza kuweka mkono kiunoni katika Salah.

MAMBO YANAYOHARIBU SALAH

1. Kuzungumza, hata kwa maneno machache huharibu Salah.
2. Kutokielekea qibla kwa kiwiliwili huharibu Salah.
3. Vyote vivunjavyo udhu huharibu Salah.
4. Harakati nyingi za mfululizo zisizo na dharura huharibu Salah.
5. Kucheka japo kidogo huharibu Salah.
6. Salah huharibika kwa kuongeza kwa makusudi tendo mionganoni mwa matendo ya Salah kama vile rukuu, au sijda, n.k.
7. Salah huharibika kwa kumtangulia imamu makusudi katika matendo ya Salah.

YANAYOKHUSU HUKUMU ZA SIJDA YA SAHAU KATIKA SALAH

1. Katika Salah yake mtu akisahau akaongeza rukuu au sijda au jalsa au akasimama; basi atakapoikamilisha Salah yake kwa kutoa salamu mbili itambidi asujudu sijda mbili ambazo ni za kufidia kusahau kwake kisha atoe tena salamu. Mfano: kama alikuwa akisali Adhuhuri, lakini

akasimama kwa ajili ya rakaa ya tano kisha akakumbuka au akakumbushwa, hapo itambidi arudi chini bila *takbir*, ambapo atakaa asome *tashahhud* ya mwisho, atoe salamu, asujudu sijda mbili za sahau na mwishowe atoe tena salamu.

Na atakiwa kufanya hivyo hivyo, asipotambua kuwa sasa yuwasali rakaa ya ziada, na akumbuke baada ya kusali hiyo ya ziada: yaani atasujudu sijda mbili za sahau kisha atatoa salamu.

2. Kama akitoa salamu kwa kusahau kabla ya kuikamilisha Salah yake, kisha akakumbuka au akakumbushwa mara tu baada ya kutoa salamu na bila kupita muda, basi atalazimika tu kukikamilisha kile alichokiacha, kisha atatoa salamu, kisha atasujudu sijda mbili za sahau na mwishowe atatoa salamu.

Mfano:

Ikiwa asali Salah ya adhuhuri akasahau akatoa salamu katika rakaa ya tatu, kisha akakumbuka au akakumbushwa, hapo awajibika kuisali rakaa ya nne na kutoa salamu, kisha asujudu sijda mbili za sahau na mwishowe atoe tena salamu. Lakini iwapo hatakumbuka ila baada ya kitambo kirefu, basi katika hali hiyo atalazimika kuirudia Salah yote toka mwanzo.

3. Kama hataisoma *Tashahhud* ya mwanzo au mfano wake miongoni mwa nyajibu za Salah kwa kusahau, basi atasujudu sijda mbili za sahau kabla ya kutoa salamu na wala hatakuwa na lawama. Akiukumbuka upungufu huo kabla ya kupaacha pahala pake, basi atalitenda alilolipunguza na wala hatakuwa na lawama. Na kama akiukumbuka upungufu huo baada ya kupapita mahali pake na kabla ya kukifikia kitendo kifuatiacho, basi atarudi akilete hicho alichokipunguza kwa kusahau.

Mfano:

Akisahau *Tashahhud* ya mwanzo akasimama kuiende~~a~~ rakaa ya tatu hadi akawa amesimama wima kikamilifu, basi katika hali hiyo harudi chini kwa ajili ya hiyo *Tashahhud* ya mwanzo, ila atalazimika mwishoni mwa Salah kusujudu sijda mbili za sahau kabla ya salamu. Na akikaa kwa ajili ya hiyo *Tashahhud* ya mwanzo lakini akasahau kuisoma kisha akakumbuka kabla ya kusimama, basi na aisome hiyo *Tashahhud* kisha aikamilishe Salah kama kawaida na hana neno. Na hivyo hivyo lau asimama bila ya kuka kwa ajili ya hiyo *Tashahhud* ya mwanzo lakini akakumbuka kabla ya kuwa amesimama wima kwa ukamilifu, basi atarudi chini na kuisoma hiyo *Tashahhud* ya mwanzo.

zo na kisha aikamilishe Salah yake kama kawaida. Lakini wamesema baadhi ya wanazuoni kuwa awajibika kusujudu sijda mbili za sahau kwa sababu ya kule kusimama kwake' kimakosa ambako kulikuwa ni ziada katika Salah yake, na Mungu ndie Ajuaye zaidi.

4. Akiitilia shaka Salah yake kuwa je, amesali rákaa mbili au tatu, wala halimbainikii moja ya hayo kuwa ni sahihi, basi ategemee kuliko na yakini, nako ni kule kufikiri kuwa amesali rakaachache: yaani mbili, kisha aikamilishe Salah yake, na asujudu sijda mbili za sahau kabla ya salamu, na mwishowe atowe salamu.

Mfano:

Ikiwa mtu asali Adhuhuri, akajiwa na shaka katika rakaayapili kuwa je, hii ni ya pili au ya tatu, wala lisimbainikie lililo sahihi kati ya hayo, basi naafikirie kuwa hiyo ni ya pili, kisha akamilishe kilichobaki, kisha asujudu sijda mbili za sahau kabla ya salamu, na mwisho atoe salamu.

5. Akiitilia shaka Salah yake, kuwa je, amesali rakaamibili au tatu, kisha likambainikia mojawapo; basi atakamilisha kilichobakiatokeahapo, kisha asujudu sijda mbili za sahau baada ya salamu na mwishowe atowe salamu.

Mfano:

Ikiwa asali Adhuhuri akajiwa na shaka katika rakaayapili kuwa je, hii ni rakaayapili au ya tatu, kisha ikambainikia kuwa hiyo ni ya tatu, basi naye aifanye kuwa ni ya tatu kisha akamilisherakaamoja iliyobaki, atoe salamu, kisha asujudu sijda mbili za sahau, na mwishowe atoe salamu.

Na kama shaka itamjia baada ya kuimaliza Salah, basi asijali inapokuwa ni yakini na sio shaka tupu.

Na ikiwa yeye ni mtu mwenye wingi wa shaka, basi asijali shaka yake hiyo, kwani yatokana na wasiwasi tu.

Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi kuliko wote. Na rehema na amani ya Mwenyezi Mungu imshukie Mtume wetu Muhammad na Aali zake na Sahaba zake.

Anavyojitaharisha Mgonjwa

1. **Mgonjwa anawajibika kujitaharisha kwa maji: atawadhe kuondoa hadathi ndogo; na aoge kuondoa hadathi kubwa.**
2. **Kama hawezi kutumia maji kwa vile hayawezi au kwa kukhofia kuwa yatamzidishia maradhi yake, au yatachelewesha kupona kwake, basi atayammam.**
3. **Jinsi ya kutayammam: Apige kwa viganja vyake pigo moja kisha apake uso wake kwa mikono yake miwili, kisha aipakaze mikono yake miwili: kwanza wa kushoto uupakaze wa kulia, kisha wa kulia uupakaze wa kushoto.**
4. **Na asiyeweza kutawadha yeze mwenyewe basi atawadhishwe au atayammamishwe na mtu mwengine.**
5. **Kama katika baadhi ya viungo vya udhu kuna jaraha basi aoshe kwa maji, lakini kama kuosha kwa maji kutadhuru basi apake tu kwa mkono wenyewe unyevunyevu wa maji, na kama kupaka huko pia kutadhuru basi atayammam.**
6. **Ikiwa katika baadhi ya viungo vyake kuna mvunjiko uliofungwa kwa kitambaa au kitata (*Plaster of Paris*), basi mahali hapo apapakaze tu kwa mkono wenyewe unyevunyevu wa maji badala ya kupaosha na wala hahitaji kutayammam kwani kupakaza huko ni badili ya kuosha.**
7. **Yajuzu kutayammam kwa kupiga kwa viganja vyake juu ya ukuta, au kitu chochote chengine tahiri chenye vumbi. Na kama ukuta au kiambaza kimepakazwa kitu chengine kama vile rangi basi asiutumie ukuta kama huo unapokuwa hauna vumbi.**
8. **Kama haiwezekani tayammam kwa kutumia vumbi la ardhi, ukuta au kitu chochote kile chenye vumbi, basi itamtosheleza kuweka mchanga kwenye chombo au kitambaa cha mkono kisha autumie mchanga huo kufanya tayammum.**
9. **Akitayammam kwa ajili ya Salah, basi hubakia na tahara yake hadi wakati wa Salah nyengine, na hiyo ataaisali kwa tayammum ya Salah ya kwanza, wala halazimiki kutayammam upya kwa ajili ya Salah hiyo ya pili, kwa vile yeze angali na tahara yake na hajapakitana na la kuitengua.**

10. Mgonjwa awajibika asaliye nguo tahiri na zinaponajisika, ni wajibu kuzifua au kuzibadilisha na kuvaan ziliizo tahiri, lakini akishindwa kabisa kufanya hivyo, basi asali katika nguo hizo hizo, na Salah yake ni sahihi wala hawajibiki kuirudia baadaye.
11. Awajibika mgonjwa kusali juu ya kitu (kama vile msala) tahiri. Na kitu hicho kikinajisika, basi ni wajibu kukiosha au kukibadilisha kwa kilicho tahiri, au kitandikwe juu yake kitu tahiri. Na asipoyaweza hayo, atasalia hicho hicho, na Salah yake ni sahihi wala hawajibiki kuirudia.
12. Haimjuzii mgonjwa kuiakhirisha Salah kwa kushindwa kujitaharisha (yaani kutawadha au kutayammam), bali ajitahirishe kwa mujibu wa uwezo wake, kisha aisali Salah kwa wakati wake, hata kama kutakuwa juu ya mwili wake, nguo zake au mahala pa kusalia najisi ambayo hamudu kuiondoa.

JINSI MGONJWA ASALIVYO

1. Awajibika mgonjwa kusali wima hata kama ni kwa kuinama au kwa kuegemea ukuta au fimbo inayomsaidia kusimama.
2. Kama akishindwa kusimama, basi asali hali amekaa vizuri chini.
3. Akishindwa kusali kikalie, basi asali hali amelalia ubavu wake huku ameelekea qibla, na ubavu wa kulia ni bora zaidi. Akishindwa kuelekea qibla, basi asali na hali ameelekea kokote, na Salah yake ni sahihi wala hatalazimika kuirudia baadaye.
4. Na akishindwa kusali juu ya ubavu wake, basi asali chali huku miguu yake imeelekea qibla, na ni bora kukiinua kidogo kichwa chake ili awe ameelekea qibla. Na kama akishindwa kuielekeza miguu qibla, basi asali na hali imeelekea kokote, na wala halazimiki kuirudia Salah yake baadaye.
5. Mgonjwa awajibika kurukuu na kusujudu katika Salah yake, akishindwa basi ataziashiria kwa kichwa chake, na ishara ya sijda iwe ya kichwa kuinama zaidi kuliko ishara ya rukuu. Na akiweza kusujudu lakini akashindwa kurukuu, basi atasujudu pa kusujudu na ataashiria pa kurukuu.
6. Akishindwa kuashiria rukuu na sijda kwa kichwa chake, basi ataashiria kwa macho yake, kwa kuyafumba kidogo kwa rukuu na zaidi kwa

sijda. Ama kule kuashiria kwa vidole—kama wafanyavyo baadhi ya wagonjwa, huko si sahihi, wala sijasikia kama kufanya hivyo kunatokana na Qur’ani au Sunnah au wala kauli za wanazuoni.

7. Na kama hawezি kuashiria kwa kichwa au kwa macho yake, basi atafanya hivyo kwa moyo wake: ataleta *takbir*, atasoma (Al-Fatiha na Sura nyengine) kisha atanua rukuu au sijda, na ‘kusimama au kukaa kwa moyo wake, na mja hulipwa kwa mujibu wa nia yake.
8. Awajibika mganjwa kusali kila Salah kwa wakati wake, na ayafanye yale yote yanayomlazimu kuyafanya kwa kadri ya uwezo wake. Lakini ikimuia vigumu kuisali kila Salah kwa wakati wake, basi aruhusiwa kujumuisha Salah ya Adhuhuri na Alasiri, na Magharibi na ‘Isha. Azijumuushe *jam ‘ut-taqdim* (yaani asali Adhuhuri na Alasiri: zote wakati wa Adhuhuri) au *jam ‘ut-ta’khir* (yaani asali Adhuhuri na Alasiri: zote wakati wa Alasiri). Na hivyo hivyo kwa Salah za Magharibi na ‘Isha. Achague lililo sahali kwake. Ama Salah ya Alfajiri haijumuishwi na Salah yoyote, bali husaliwa peke yake.
9. Kama mganjwa ni msafiri, mathalan yuko katika matibabu mbali na kwao, basi aruhusiwa kuzifupisha zile Salah za rakaa nne nne azisali rakaa mbili mbili; nazo ni Adhuhuri, Alasiri na ‘Isha mpaka atakapdrudi kwao, iwe kwa muda mfupi au muda mrefu.

Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kutoa tawfiqi.

Imeandikwa na fiqiri kwa Mwenyezi Mungu:
Muhammad As-Salih Al-‘Uthaimin.